# JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI
# SHULE YA SEKONDARI LANGASANI.

**Namba za simu:**
0715 994677 Mkuu wa shule
0759618493 Makamu mkuu wa shule
0629 771624 Makamu mkuu wa shule.

**SHULE YA SEKONDARI LANGASANI,**
**S.L.P 158**,
**MOSHI**.
31/03/2022

**KUMB. NA.LSS/ _____**
**MZAZI/ MLEZI WA _____**

**YAH: <u>MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO 2022/2023 SHULE YA SEKONDARI LANGASANI.</u>**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa mwanao _____amebahatika kuchaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano 2022/2023 katika shule ya sekondari Langasani, **HONGERA SANA**. Shule hii ipo ndani ya eneo la kiwanda cha sukari **TPC** mkoa wa Kilimanjaro, wilaya ya Moshi na umbali wa takribani **25km** toka Moshi mjini.

Shule itafunguliwa tarehe __/__2022 na masomo yataanza rasmi tarehe__/__2022 saa moja na nusu asubuhi. Mwanao aje na mahitaji yote ya shule kama ifuatavyo:-

**KUNDI A: ADA NA MICHANGO YA SHULE**

| | | MUHULA WA KWANZA | MUHULA WA PILI |
|---|---|---|---|
| 01 | Ada ya shule | Tsh . 35,000/= | Tsh 35,000/= |
| 02 | Tahadhari | Tsh . 5,000/= | |
| 03 | Taaluma | Tsh. 10,000/= | Tsh 10,000/= |
| 04 | Wahudumu (walinzi, wapishi, matrone n.k) | Tsh . 25,000/= | Tsh 25,000/= |
| 05 | Ukarabati wa samani | Tsh. 15,000/= | |
| 06 | Matibabu ya huduma ya kwanza | Tsh. 10,000/= | Tsh 10,000/= |
| 07 | Ujenzi wa ukuta/uzio | Tsh. 8,000 | |
| | **JUMLA** | **TSH 108,000/=** | **Tsh80,000/=** |
| | **JUMLA KUU KWA MWAKA** | **TSH 1880000/=** | |

*NB: Ada na michango yote ilipwe kwenye akaunti NA: **40301000032 NMB** jina la akaunti ni **LANGASANI SECONDARY SCHOOL***

**CHACHA JOSEPH**
**MKUU WA SHULE**

## KUNDI B: SARE ZA SHULE.

**i.** Sketi mbili (**02**) rangi ya zambarau yenye urefu wa inchi nane toka mguuni (**muhimu sana**)
**ii.** Aje na mashati mawili meupe ya mikono mifupi, kwa waislamu yawe ya mikono mirefu.
**iii.** Sweta moja rangi ya zambarau (**ifanane na rangi ya sketi**)
**iv.** Aje na viatu vyeusi **vyenye Kamba, visigino vifupi, visiwe na mapambo na urembo wowote**
**v.** Aje na soksi rangi nyeupe **ndefu** jozi mbili
**vi.** Tai ndefu rangi ya zambararu.
**vii.** Sketi mbili nyeusi ndefu nchi nane toka miguuni (**muhimu sana**) na t shirt mbili (02) nyekudu **round collar** zisizo na maandishi kwa ajili ya kushindia.

Kwa waislamu **hijabu** na "*vya kuvalia ndani ya hijabu*" ni rangi **nyeupe tu**, zisizo na urembo wowote. **Hijabu iwe ndefu inayofunika mikono yote.** Atavaa awapo darasani na hata katika sare ya kushindia.

**viii.** Aje na track suti rangi ya bluu kwa ajili ya kuvaa wakati wa kujisomea usiku.
**ix.** **SARE ZA MICHEZO:** kila mwanafunzi aje na bukta na tshirt rangi ya light blue (jezi ya Manchester city) raba nyeupe kwa ajili ya michezo.

## KUNDI C: VIFAA

### I. VIFAA BINAFSI:

Godoro la inchi $3^{1}/_{2}$ x 6, Shuka 2 za rangi ya pinki, Chandarua, Ndoo ndogo ya kuogea, Sanduku dogo la chuma, ( asije na begi la nguo sanduku la chuma yaani tranka linatosha.) Mto na foronya, Torch na betri, kijiko, kikombe na sahani (container).

### II. VIFAA VYA SHULE.

| VIFAA KWA WANAFUNZI WA HGL | VIFAA KWA WANAFUNZI WA CBG |
|---|---|
| - Rim paper moja (01) **A4**<br>- Rim paper **ruled** moja (karatasi zilizopigwa mistari)<br>- Jembe lenye mpini moja<br>- Ndoo kubwa ya lita 20 - mpya.<br>- Ufagio wa chelewa wenye kishikio cha mti.<br>- Dawa za chooni lita tano (**05 ltrs)** | - Rim paper moja (01) **A4**<br>- Rim paper **ruled** moja (karatasi zilizopigwa mistari)<br>- Jembe lenye mpini moja.<br>- Ndoo kubwa ya lita 20 - mpya<br>- Ufagio wa chelewa wenye kishikio cha mti.<br>- Squizer moja.<br>- Mfagio wa buibui. |

### III. VIFAA VYA MASOMO:

Kila mwanafunzi aje na;

1. Madaftari makubwa (counter book) ya kutosha masomo yake, mazoezi na majaribio.
2. Kalamu za kutosha za wino, penseli, ufutio, stapler mashine na stapler pins.
3. Scientific Calculator.
4. **Dissecting kit** kwa mwanafunzi anayesoma somo la Baiolojia.
5. Vitabu vya masomo kwa tahasusi husika. (vimeorodheshwa uk. wa 06)

- Pia Mzazi/Mlezi unaombwa umfungulie mwano akaunti yake binafsi ya benki kwa ajili ya kumtumia pesa ya kujikimu kwa mahitaji yake mbalimbali kuepuka usumbufu wa kutuma pesa kwenye namba za simu kwa usalama wa pesa za mwanafunzi kwani shule haitawajibika na namna yoyote ya upotevu wa pesa kupitia miamala ya simu yoyote utakayotumia. Huduma za benki kama **NMB, CRDB, EQUITY** na **MKOMBOZI BANK** zinapatikana karibu na shule na ni rahisi na salama kwa matumizi ya mtoto wako. Kama anayo akaunti tayari basi endelea kuitumia ikiwa ni kwa benki zilizoorodheswa. ***(NI MUHIMU SANA)***
- Pamoja na barua hii viambatanisho vifuatavyo vimefungashwa*
  i. Kiambatanisho A: sheria za shule
  ii. Kiambatanisho B: fomu ya dakatari (medical examination form)
  iii. Kiamabtanisho C: fomu ya taarifa binafsi za mwanafunzi
  iv. Kiambatanisho D: ahadi ya mzazi/mlezi kulipa ada na michango ya shule
  v. Kiambatanisho E: ahadi ya utii na tabia njema.

**KIAMBATISHO: A**

# SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978 na inazingatia miongozo inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Aidha wanafunzi wote wanatakiwa kuzingatia haya yafuatayo:-

Kila mwanafunzi anayejiunga na shule hii anapaswa kutambua kuwa yupo hapa kwa ajili ya KUSOMA kwa faida yake, familia yake na Taifa kwa ujumla. Kwa sababu hiyo, chochote kilichopo nje ya jukumu hili hakina nafasi katika shule hii.

**Mahudhurio:**

- Kuwahi shuleni ni wajibu wa kila mwanafunzi hivyo kila mwanafunzi anapaswa kuripoti shuleni tarehe ya kufungua shule bila kukosa na kuendelea kuwepo shuleni kila siku.
- Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vipindi vyote vya darasani ndani na nje ya darasa. Vipindi vya kazi za mikono pamoja na michezo ni sehemu ya masomo.
- Ni lazima kutimiza kwa makini mahudhurio ya maandalio ya jioni (Evening preparation).
- Wanafunzi wote wanatakiwa kuhudhuria mikusanyiko halali yote ya shule kama vile, mstarini, usafi, Baraza la shule, ibada, midahalo(debates)n.k
- Kila mwanafunzi anawajibika kuwahi kula chakula kwa wakati uliopangwa. Ni marufuku kuwahi kuchukua chakula kabla ya wengine wote. Kama kuna tatizo lolote liripotiwe kwa mwalimu wa zamu/wa chakula kwanza.

**Sare za shule:**

- ❖ Wanafunzi wote ni lazima kuvaa sare za shule muda wote wa darasani na wanapotoka nje ya shule.
- ❖ Mwanafunzi lazima ajiweke katika hali ya usafi kimwili na kimavazi. Nguo zote atakazovaa mwanafunzi lazima zikubaliwe na uongozi wa shule pale anaporipoti mwanafunzi shuleni tu.
- ❖ Nguo za michezo huvaliwa wakati wa michezo tu.

**Heshima na Utii:**

- ➢ Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema popote alipo ndani na nje ya mipaka ya shule
- ➢ Kila mwanafunzi anatakiwa kutii kengele, kutii na kuwaheshimu walimu, wafanyakazi wote, Viranja wa shule na jumuiya nzima ya shule.
- ➢ Mwanafunzi anatakiwa kusimama/kumpokea na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri anapopita au aingiapo shuleni au darasani
- ➢ Wanafunzi wanatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, fedha za Taifa, Wimbo wa Taifa, Wimbo wa shule, Nembo ya Taifa na picha za viongozi wa serikali.
- ➢ Kiranja yeyote wa shule anatakiwa kula kiapo cha utii na kuwa mfano katika kutekeleza kanuni na taratibu za shule. Kukiuka taratibu za shule kunaweza kumpotezea sifa ya kuwa kiongozi na adhabu nyingine kuchukuliwa dhidi yake ikiwa pamoja na kusimamishwa/kufukuzwa shule. Mkuu wa shule ana mamlaka ya kuteua kiongozi mwingine wakati wowote pale itakapobidi.

**Sehemu muhimu za kujifunzia**:

**a.** Madarasa, Maabara na maktaba ni sehemu za masomo, hivyo ni marufuku kwa mwanafunzi kupiga kelele, kuzomea, kupiga gumzo au kuzurura ndani na sehemu hizo. Hairuhusiwi kutumia viti na madawati kusomea nje ya madarasa. Ikithibitika hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa.
**b.** Nimarufuku kuingia kwenye maabara bila ya kibali cha mwalimu husika.
**c.** Ni lazima kila mwanafunzi atumie maktaba kufuatana na sheria za maktaba.

**Afya**

Kila mwanafunzi lazima ajiweke katika hali nzuri ya kiafya ili aweze kuyamudu masomo yake vyema.

**i.** Endapo mwanafunzi ataugua ataomba ruhusa kwa mwalimu wa zamu/mwalimu mshauri wa wanafunzi kama ataenda hospitali na kurudi siku hiyo hiyo. Kwa wanafunzi wa bweni au hostel taratibu za matibabu zitaratibiwa na walimu wa mabweni na Ruhusa ya kulala nje ya shule itatolewa na mkuu wa shule tu.
**ii.** Gharama za matibabu zilizo nje ya bima zitagharamiwa na mzazi/mlezi wa mwanafunzi husika.
**iii.** Mwanafunzi hatakiwi kuchafua mazingira ya shule kwa namna yoyote ile mfano kutupa taka ovyo, kwenda haja kubwa na ndogo mahali pasipostahili n.k
**iv.** Mwanafunzi anapaswa kutunza mwili wake ikiwa ni pamoja na kukata kucha, kunyoa nywele na ndevu, kutandika kitanda, kuoga kupiga mswaki, na kupanga vitu vizuri bwenini n.k

**Mipaka ya shule;**

- Mwanafunzi yeyote atakae toka nje ya mipaka ya shule lazima apate kibali cha mwalimu wa zamu na awe amevaa sare ya shule. Kwa wanafunzi wa bweni au hostel kibali maalum ni lazima kisainiwe na mkuu wa shule.
- Ni marufuku kwa mwanafunzi kutembelea sehemu zifuatazo:- vilabu vya pombe, majumba ya starehe na nyumba za kufikia wageni.

**Vifaa na mali za shule:**

- Majengo ya shule, samani, vifaa vya kazi na vifaa vya masomo ni mali inayogharimu Fedha nyingi sana, hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kuvitunza vizuri ili viweze kudumu kwa manufaa ya badaye.
- Ni marufuku kuandika au kuweka alama/chata katika kuta, milango, madirisha, meza au dawati au kiti na vitu vingine ambavyo ni mali ya shule.
- Ni wajibu wa kila mwanafunzi kutoa taarifa kwa kiongozi/mwalimu mara tu uharibifu/kuvunja kifaa chochote cha shule unapotokea.
- Uharibifu wowote au upotevu wa kitu chochote cha shule lazima ufidiwe.
- Mali zote za shule utakazokabidhiwa utalazimika kuzirudisha zikiwa katika hali nzuri vinginevyo utalipia uharibifu.

## MAKOSA AMBAYO YANAWEZA KUMFUKUZISHA SHULE MWANAFUNZI.

i. Kumiliki au kukutwa na simu ya mkononi au laini. Ikikamatwa kwanza itaharibiwa kabisa na pia hatua nyingine kuchukuliwa ikiwemo kufukuzwa shule.
ii. Wizi.
iii. Uasherati/ubakaji/ushoga au vyote kwa pamoja.
iv. Ulevi wa aina yeyote au uvutaji wa sigara, bangi na madawa ya kulevya na kucheza kamari.
v. Kupiga au kupigana.
vi. Kugoma(mfano kutokula chakula cha shule), kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule na watu.
vii. Kuharibu kwa makusudi mali ya shule/umma.
viii. Kumpa mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule pamoja na kupata mimba au kuharibu (kutoa mimba) ndani na nje ya shule.
ix. Kuoa au kuolewa
x. Kudharau Bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa, Fedha za Taifa, Wimbo wa Taifa au picha za viongozi wa serikali.
xi. Utoro wa shule, mahudhurio mabovu darasani au kukosa kufanya mitihani/majaribio/mazoezi bila taarifa au kibali maalum cha mkuu wa shule
xii. Kufanya makosa mengine ya jinai au uhaini kama vile kumiliki Baruti, silaha za moto na mfano wa hayo.
xiii. Kukataa adhabu ya mwalimu,kugomea au kumtukana mwalimu au mtu yeyote.
xiv. Kuchelewa kufika shule, au kukosa kuwepo shuleni kwa siku 90 mfululizo bila taarifa rasmi.



NB: **Shule haina vitabu vya kutosheleza, hivyo mzazi mnunulie mwanao baadhi ya vitabu atakavyohitaji mfano wa vitabu hivyo vimeorodheshwa katika jedwali lifuatalo;**

## ORODHA YA VITABU

| Na. | SOMO | JINA LA KITABU |
|---|---|---|
| 1. | ENGLISH LANGUAGE | - Oxford Advanced Learner's Dictionary<br>- Advanced Level English: A Practical Aproach. Nicholaus Asheli,Good Book Publishers<br>- Literature for advanced level: Godfrey Ruta Bukagile.Nyambari Nyangwine Publishers<br>- English for A level - Oxford<br>- English For Form 5&6 Phonology Part II; Michael Kadeghe.<br>- Complete English Course For Form 5&6 students; Michael Kadeghe<br>- Advance Level English Language , PP II ( Novel Questions and Answers; Nyambari Nyangwine |
| 2. | HISTORY | - Mastering Modern World History- Norman Lowe<br>- How Europe Underdeveloped Africa-Walter Rodney<br>- Problems and Prospective in History; Social Changes and Revolution in England 1540-1640; Lawrence Stone<br>- Adv. Level History Qns and Ans; Nyambari Nyangwine<br>- The Origins and Development of Africa societies selected Qns and Ans; Nyambari Nyangwine<br>- A History Modern Europe 1789-1981; H. L. Peacock |
| 3. | GEOGRAPHY | - Integrated Approach to Physical Geography (Msabila)<br>- Integrated Geography (By F. J. Monkhouse)<br>- Map reading for East Africa<br>- Principles of Geography (By F.J. Monk house)<br>- General Geography in diagram (By R.P. Bunnet)<br>- Simplified Physical Geography for a level (By D.M.Mapunda)<br>- Practical Geography For Africa (Longman 1983) J. M. Pritchard<br>- Atls For Secondary schools; Longman Group<br>- Geography, An Intergrated Approach; D. Waugh<br>- An Integrated Focal Reginal Studies on Human Economic Geography; A-Level PP 1&2 D. T. Msabila |
| 4. | BIOLOGY | - Biological Science,3rd Ed Green; Cambridge<br>- Understanding Biology<br>- Advance d Biology<br>- Functional Approach. MBU Robert; 4th Ed. |
| 5. | CHEMISTRY | - Organic Chemistry Volume I<br>- Advanced level Inorganic chemistry Part I & II (TIE 1995)<br>- Advanced Chemistry review by William W. Davis (Mzumbe Book Project 2004)<br>- Physical Chemistry by Delungu (Mzumbe Book Project, 1998)<br>- Chemistry in Action; Freementle M<br>- A-Level Physical Chemistry ; Heys 6th Edition<br>- A-Level Chemistry; E.N Ramsed |
| 6. | BAM | - Basic applied mathematics by Wakamoga Masinde<br>- Basic Applied Mathematics by gdy publication. |

**KIAMBATISHO: B**

**BANDIKA PICHA (PASSPORT SIZE) YA MWANAFUNZI HAPA**

# TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI.

JINA KAMILI: _____

TAREHE YA KUZALIWA: _____

KABILA: _____

MKOA ALIPOZALIWA: _____

WILAYA ALIYOZALIWA: _____

JINA LA MZAZI: _____

KAZI YA MZAZI: _____

ANWANI YA MZAZI: _____

SHULE YA MSINGI ALIYOTOKEA MWANAFUNZI NA ANWANI:
_____

SIMU NA ANWANI YA NDUGU WA KARIBU WAKATI WA DHARURA: _____

UHUSIANO WAKE NA MWANAFUNZI: _____

TATIZO LA KUDUMU LA KIAFYA KAMA LIPO, MZIO AU ALLERGY (***Lithibitishwe na VIPIMO vya daktari katika fomu ya daktari***): _____
_____

WAZAZI WAPO PAMOJA AU WAMETENGANA: _____

MAMA YUPO HAI? _____

BABA YUPO HAI? _____

JINA LA ANWANI AMBAPO TAARIFA ZA MWANAFUNZI ZITATUMWA:
_____

SAINI YA MWANAFUNZI: _____

TAREHE: _____

SAINI YA MZAZI: _____

TAREHE: _____

**MKONDO NA DARASA ALIPOPANGIWA MWANAFUNZI: _____**

**SAINI YA MWALIMU WA DARASA: _____**

**SAINI YA MKUU WA SHULE: _____**

**TAREHE: _____**

**KIAMABATISHO: C**

**PRRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION LOCAL GOVERNMENTS**
**MOSHI DISTRICT COUNCIL**

**LANGASANI SECONDARY SCHOOL,**
**P.O. BOX 158,**
**LANGASANI – MOSHI.**

**Date** ----------

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM.**

**TO THE MEDICAL OFFICER.**
_____
_____
_____

Please ---------- (name of the student) who has been selected to join this school for his/her fitness as a student in the following areas (to be completed by a medical officer)

1. Eye sight ----------
2. Hearing ----------
3. Tuberculosis (T.B) ----------
4. Specimen ----------
   i. Stool ----------
   ii. Urine ----------
   iii. Blood ----------
5. Asthma ----------
6. Pregnancy ----------
7. Other diseases/ any disabilities ----------

**MEDICAL CERTIFICATE.**

(To be completed by medical officer.)

I have examined the above named and consider that he/ she is physically not physically fit as a student.

***Date*** ---------- ***Signature*** ----------

***Station*** ---------- ***Designation*** ----------

***Official stamp***----------

***NB:*** ***I request this form to be returned to the school in a sealed envelope***

**KIAMBATISHO: D**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI.**
**SHULE YA SEKONDARI LANGASANI**

## AHADI YA MZAZI YA KUMUHUDUMIA MTOTO KWA KILA JAMBO SHULE ITAKALOELEKEZA.

Mimi _____ Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi _____ wa kidato cha _____ Ninakubali/Sikubali kuwa mtoto wangu ajiunge na shule ya sekondari Langasani kuanzia leo tarehe _____ na naahidi kuwa nipo tayari kumuhudumia mtoto kwa kila jambo litakaloelekeza shule.

Aidha naahidi kuwa ifikapo kila mwisho wa robo muhula nitakuja kufuatilia maendeleo ya mwanangu shuleni (nitakuja shuleni mara nne kwa mwaka ili kufuatilia maendeleo ya mwanangu kitaaluma) na mtoto wangu ameahindi mbele yangu kuwa atakuwa mtiifu na mwenye bidii awapo shuleni.

Ninatambua uwepo wa dini mbalimbali, na nikiwa kama Mzazi/Mlezi ninapenda mtoto wangu akiwa shule alelewe katika dini ya _____ dhehebu _____

**Jina la mzazi/mlezi _____ Sahihi _____**

**Anuani _____ simu No: _____**

**Tarehe _____**

**N.B:** ***Futa isiyo sahihi.***

**KIAMBATISHO: E**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI.**
**SHULE YA SEKONDARI LANGASANI**

# AHADI YA UTII /TABIA NJEMA.

Mimi _____ (*majina matatu ya mwanafunzi*) ninayejiunga kidato cha _____ katika shule ya sekondari Langasani, natambua vyema wajibu wangu kwa taifa kama mwanafunzi, kwa hiyo naahidi mbele ya Mzazi/Mlezi wangu na mbele ya Mkuu wa shule kuwa:-

a. Nitafuata sheria na kanuni zote za shule pamoja na maelekezo yote halali yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.
b. Nitatii na kuwaheshimu walimu, watumishi wasio walimu viongozi wangu wote kuanzia ngazi ya viranja wa madarasa,viranja wa shule hadi mkuu wa shule.
c. Na kama nitashindwa kufuata/kuzingatia maadili mema nipewayo na walimu wangu shuleni hatua kali zitachukuliwa dhidi yangu ambayo ni pamoja na kufukuzwa shule.

**Ahadi hii imetolewa leo siku ya _____ Tarehe _____**

**_____** **_____**
**Jina la mwanafunzi** **Saini ya Mwanafunzi**

**_____** **_____**
**Jina la mzazi/mlezi** **Saini ya Mzazi/Mlezi**

**Maoni ya mkuu wa shule: _____**
**_____**

**Tarehe: _____** **Saini ya Mkuu wa Shule.** **_____**